# TANZANIA ELECTION MONITORING COMMITTEE (TEMCO)

REDET - LEAD AGENCY OF TEMCO

**TAARIFA YA AWALI KUHUSU UBORESHAJI WA DAFTARI LA KUDUMU LA WAPIGA KURA**

*Imetolewa na*
*Kamati ya Uangalizi wa Chaguzi Tanzania (TEMCO)*

**MACHI 2020**

# YALIYOMO

YALIYOMO ..... ii
ORODHA YA VIFUPISHO ..... iii
1. UTANGULIZI ..... 1
2. METHODOLOJIA ..... 1
3. ELIMU YA MPIGA KURA ..... 3
4. UPATIKANAJI NA MAFUNZO KWA MAAFISA WAANDIKISHAJI ..... 7
4.1 Upatikanaji wa Maafisa Waandikishaji ..... 7
4.2 Mafunzo kwa Maafisa Waandikishaji ..... 8
5. MCHAKATO WA KUANDIKISHA WAPIGA KURA ..... 9
5.1 Ufunguzi wa Vituo vya Kuandikisha Wapiga Kura na Utoshelevu wa Vifaa ..... 9
5.2 Utoshelevu wa Vifaa vya Kuandikishia ..... 10
5.3 Mipango ya Kiusalama ..... 11
5.4 Ufanisi wa Maafisa Waandikishaji ..... 12
5.5 Utendaji Kazi wa Mashine za BVR na Uandikishaji wa Wapiga Kura ..... 13
5.6 Mahali na Urahisi wa Kuvifikia Vituo vya Kuandikisha Wapiga Kura ..... 16
5.7 Ushiriki wa Vyama vya Siasa ..... 20
5.8 Kushirikiana na Waangalizi wa TEMCO ..... 21
5.9 Kufunga Vituo vya Kuandikisha Wapiga Kura ..... 21
6. HITIMISHO NA MAPENDEKEZO ..... 22
6.1 Hitimisho ..... 22
6.2 Mapendekezo ..... 24
KIAMBATISHO I: MAENEO AMBAYO UANGALIZI WA TEMCO ULIFANYIKA ..... 26

## ORODHA YA VIFUPISHO

| | | |
|---|---|---|
| ACT-Wazalendo | - | Action for Change and Transparency-Wazalendo |
| ARO | - | Assistant Registration Officer |
| BVR | - | Biometric Voter Register |
| CCM | - | Chama cha Mapinduzi |
| CHADEMA | - | Chama cha Demokrasia na Maendeleo |
| CSO | - | Civil Society Organization |
| CUF | - | Civic United Front |
| DC | - | District Council |
| ID | - | Identity Card |
| IT | - | Information Technology |
| LGA | - | Local Government Area |
| MC | - | Municipal Council |
| NCCR-Mageuzi | - | National Convention for Construction and Reform-Mageuzi |
| NEC | - | National Electoral Commission |
| PNVR | - | Permanent National Voters' Register |
| PWD | - | People with Disabilities |
| RO | - | Registration Officer |
| TEMCO | - | Tanzania Election Monitoring Committee |

## 1. UTANGULIZI

Hii ni taarifa ya awali iliyoandaliwa na Tanzania Election Monitoring Committee (TEMCO) kuhusu uboreshaji wa daftari la kudumu la wapiga kura (PNVR) uliofanywa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC). Ibara ya 74(6) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeipa Tume jukumu la kusimamia na kuratibu uandikishaji wapiga kura kwa ajili ya uchaguzi wa rais, wabunge na madiwani katika Jamhuri ya Muungano. Zoezi la uboreshaji wa daftari la kudumu la wapiga kura ni sehemu muhimu ya maandalizi ya uchaguzi mkuu utakaofanyika mwezi Oktoba 2020. Uboreshaji wa daftari hilo ulihusisha shughuli kuu nne, uandikishaji wapiga kura wapya ambao wametimiza umri wa miaka 18 na wengine ambao watafikisha umri huo mwezi Oktoba. Ulihusisha pia watu ambao wamehamia maeneo mengine ya makazi na walipenda kuamishia taarifa zao huko. Zoezi hili lilitoa fursa kwa wapiga kura ambao vitambulisho vyao vimeharibika au kupotea kupata vitambulisho vipya. Mwisho, zoezi la kuandikisha wapiga kura lilihusisha kuwaondoa kutoka kwenye daftari la kudumu la wapiga kura watu waliopoteza sifa za kuwa wapiga kura, kama watu waliofariki.

Tangu zoezi la uboreshaji wa daftari la kudumu la wapiga kura lianze tarehe 18 Julai 2019 mikoa 26 ya Tanzania Bara na mikoa 5 ya Zanzibar tangu zoezi lilipozinduliwa rasmi tarehe 18 Julai, 2019 mkoani Kilimanjaro. Kwa mujibu wa kifungu cha 40(1) cha Kanuni za Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura (zilizochapishwa kwenye Gazeti la Serikali Namba 792 na 793 tarehe 28 Desemba 2018) na kifungu cha 42(1) cha Kanuni za Serikali za Mitaa za Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura za mwaka 2018, Tume iliialika TEMCO kuangalia zoezi la uboreshaji wa daftari la kudumu la wapiga kura. TEMCO ilianza kuangalia uboreshaji wa daftari la kudumu la wapiga kura tarehe 1 Desemba 2019 na ilifanya kazi hiyo kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa 89 katika mikoa 16 ya Tanzania Bara na Zanzibar.

Kwa mantiki hiyo, taarifa hii inajumuisha mikoa 16 ya Tanzania, pamoja na mikoa mitano ya Zanzibar, Mamlaka 89 za Serikali za Mitaa na vituo 614 vya kuandikisha wapiga kura. Taarifa hii imegawanyika katika sehemu sita, pamoja na utangulizi. Sehemu ya pili inajikita kwenye methodolojia. Sehemu ya tatu inahusu utoaji wa elimu ya mpiga kura. Sehemu ya nne inaangalia upatikanaji na utoaji mafunzo kwa maafisa walioandikisha wapiga kura. Mchakato wa kuandikisha wapiga kura unatazamwa katika sehemu ya tano ya taarifa hii. Sehemu ya sita inatoa hitimisho na mapendekezo.

## 2. METHODOLOJIA

Kati ya 1 Desemba 2019 and 18 Januari 2020, TEMCO ilipeleka waangalizi 89 kwenye vituo 614 vya kuandikisha wapiga kura katika Mamlaka 89 za Serikali za Mitaa kwenye mikoa 16 ya Tanzania Bara na Zanzibar. Tume iliendesha zoezi la uboreshaji wa daftari

la kudumu la wapiga kura kwa awamu, ikifanya hivyo kwenye makundi ya mikoa au kanda kwa muda fulani. Mpango wa uangalizi wa TEMCO (tazama Kiambatisho I) ulifuata mchakato wa Tume kwa awamu ambao uligawanyika katika kanda tano, yaani:

(i) Kanda ya Kati: Dodoma (Mkoa 1);
(ii) Kanda ya Pwani: Dar es Salaam, Pwani, Morogoro na Tanga (Mikoa 4);
(iii) Kanda ya Kusini: Lindi, Mtwara na Ruvuma (Mikoa 3);
(iv) Kanda ya Nyanda za Juu Kusini: Iringa, Mbeya na Njombe (Mikoa 3); na
(v) Kanda ya Zanzibar: Kaskazini Pemba, Kaskazini Unguja, Kusini Pemba, Kusini Unguja na Mjini Magharibi (Mikoa 5).

Kila mwangalizi wa TEMCO alipewa orodha ya kuangalia awamu mbili za uboreshaji wa daftari la kudumu la wapiga kura kwa ajili ya uchaguzi wa mwaka 2020. Kwanza, aliangalia shughuli zilizofanywa kabla ya zoezi la kuandikisha wapiga kura kuanza kwa muda wa siku tatu hadi kipindi cha uandikishaji. Orodha ya shughuli zilizoangaliwa kabla ya zoezi la kuandikisha wapiga kura kuanza ilikuwa na maswali kuhusu utoaji wa elimu ya mpiga kura, utoaji wa mafunzo kwa maafisa waandikishaji wapiga kura na mazingira ya ujumla ya mahali ambapo zoezi la kuandikisha wapiga kura lilifanyika. Orodha ya kuangalia shughuli za maandalizi ya kuandikisha wapiga kura iliwasilishwa siku ya tatu, siku moja kabla ya siku ya kuandikisha wapiga kura katika Mamlaka za Serikali za Mtaa.

Pili, TEMCO iliangalia zoezi la kuandikisha wapiga kura kwa muda wa siku saba kama ilivyoelekezwa na Tume. Katika kipindi hiki, waangalizi wa TEMCO walitembelea vituo vya kuandikisha wapiga kura vilivyokuwa kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa za maeneo yao ya kazi, kituo kimoja kwa siku kuanzia saa mbili asubuhi. Waangalizi walipaswa kutoa ripoti za kila siku kwa kila kituo cha kuandikisha wapiga kura walichotembelea. Orodha ya vituo vya kuandikisha wapiga kura ilikuwa na maswali kuhusu maandalizi, taratibu za kuandikisha wapiga kura na ufungaji wa vituo.

Pia, waangalizi wa TEMCO walituma taarifa juu ya matukio makubwa kwenye kanzidata ya TEMCO. Walitoa taarifa juu ya matukio waliyoyashuhudia moja kwa moja na waliyoyasikia kupitia vyanzo vingine vya kuaminika. Taarifa kutoka kwenye vyanzo vingine zilithibitishwa kwa kutumia mchakato wenye hatua nne. Kwanza, waangalizi wa TEMCO walitathmini kama chanzo cha taarifa ni cha kutegemewa, kuaminika na kisicho na upendeleo. Pili, waliangalia kama matukio yaliyoripotiwa yangeweza kuwa yametokea. Tatu, waangalizi walithibitisha matukio hayo kwa kutumia vyanzo vingine kama vyombo vya habari, wananchi wengine na maafisa wa kuandikisha wapiga kura. Mwisho, na ilipowezekana, waangalizi wa TEMCO waliimizwa kupata ushahidi halisi ili kuongezea taarifa zao. Ingawa matukio yaliangaliwa kupitia vyanzo vingine, inapaswa ieleweke kwamba taarifa juu ya matukio hayo ni tofauti na matukio yaliyoangaliwa moja

kwa moja. Lakini, taarifa kutoka vyanzo hivyo iliwawezesha waangalizi wa TEMCO kutoa picha ya kina zaidi juu ya matukio yaliyojitokeza katika Mamlaka za Serikali za Mitaa katika kila kipindi cha kutoa taarifa husika.

Waangalizi wote wa TEMCO waliidhinishwa na Tume na walipewa mafunzo ya kina kwa muda wa siku mbili kuhusu sheria na kanuni za kuandikisha wapiga kura, kanuni za maadili ya kutopendelea upande wowote, uelewa wa hojaji za uangalizi na utaratibu wa kuwasilisha taarifa.

## 3. ELIMU YA MPIGA KURA

Ripoti za waangalizi wa TEMCO kutoka Mamlaka 89 za Serikali za Mitaa zinaonesha kwamba kwa ujumla zoezi la utoaji elimu ya mpiga kura liliendeshwa katika mazingira ya amani. Hakuna vitendo vyovyote vya kuwabughudhi au kuwatisha watoaji elimu ya mpiga kura viliripotiwa. Waangalizi wote hawakuona au kusikia chochote kuhusu kuvamiwa, kutishwa au kunyanyaswa kwa watoaji elimu ya mpiga kura, maafisa waandikishaji wapiga kura au asasi za kiraia. Pia, waangalizi wa TEMCO hawakushuhudia au kusikia chochote kuhusu unyanyasaji wa wanawake, unyang'anyi au uharibifu wa vitambulisho vya wapiga kura. Kifungu 4C cha Sheria ya Uchaguzi (CAP 343 Revised Editions of 2015) kinaipa Tume jukumu la kutoa, kusimamia na kuratibu utoaji wa elimu ya mpiga kura. Tume iliidhinisha ushirikishwaji wa asasi za kiraia 12 kati ya asasi 28 zilizoomba kutoa elimu ya mpiga kura. Lakini ni asasi chache sana kati ya zile zilizoruhusiwa ambazo zilitoa elimu ya mpiga kura kwa sababu za ukosefu wa rasilimali. Waangalizi wengi wa TEMCO (asilimia 91) walisema kwamba elimu ya mpiga kura ilitolewa na Tume. Kama Jedwali Namba 3.1 linavyoonesha, waangalizi wachache sana (asilimia 21) walisikia kwamba shughuli hizo zilifanywa na asasi za kiraia kwenye mamlaka ambazo walipangiwa kufanya kazi. Vigezo vilivyotumiwa na Tume kutoa vibali ni pamoja na Asasi iliyoomba kutoa elimu ya mpiga kura:

i. Kuwa na usajili kwa mujibu wa Sheria za Tanzania;
ii. Kuwa imefanya kazi Tanzania si chini ya miezi 6 toka kusajiliwa;
iii. Miongoni mwa Watendaji wake wakuu, Wawili wanapaswa wawe Watanzania;
iv. Kuwa haina taarifa za kuvuruga amani au kuchochea fujo; na
v. Kuwa tayari kujigharamia katika kutoa Elimu ya Mpiga Kura.

**Jedwali Na. 3.1: Utoaji wa Elimu ya Mpiga Kura**

| *Swali* | *Ndiyo, nilishuhudia (%)* | *Ndiyo, nilisikia (%)* | *Hapana (%)* | *Jumla* (%) |
|---|---|---|---|---|
| Umeshuhudia au kusikia kuhusu shughuli zozote za utoaji wa elimu ya | 32 (36) | 49 (55) | 8 (9) | 89(100) |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| mpiga kura zilizofanywa na Tume katika Mamlaka ya Serikali ya Mtaa ulipofanya uangalizi? | | | | |
| Je, ulishuhudia au kusikia kuhusu shughuli za utoaji wa elimu ya mpiga kura zilizofanywa na asasi za kiraia katika Mamlaka ya Serikali ya Mtaa ulipofanya uangalizi? | 0 (0) | 19 (21) | 70 (79) | 89(100) |

Ilibainika pia kwamba ushiriki wa vyama vya siasa kwenye utoaji wa elimu ya mpiga kura ulikuwa mdogo. Waangalizi wa TEMCO walishuhudia hasa viongozi na/au makada wa CCM na kwa kiasi kidogo CHADEMA wakielimisha na kuhamasisha watu wajiandikishe (tazama Jedwali Namba 3.2).

**Jedwali Na. 3.2: Ushiriki wa Vyama vya Siasa kwenye Kuhamasisha Wapiga Kura Wajiandikishe**

| *Hakuna elimu ya mpiga kura iliyotolewa na vyama vya siasa (%)* | *CCM (%)* | *CHADEMA (%)* | *CUF (%)* | *ACT-Wazalendo (%)* | *NCCR-Mageuzi (%)* | *Vingine (%)* | *Jumla (%)* |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 57 (64) | 30 (34) | 17 (19) | 7 (8) | 6 (7) | 2 (2) | 1 (1) | 89 (100) |

Wananchi wachache walijitokeza kupata elimu ya mpiga kura. Kama Jedwali Namba 3.3. linavyoonesha, ni waangalizi wachache sana wa TEMCO (asilimia 12) walisema kwamba wananchi wengi walijitokeza kupatiwa elimu ya mpiga kura. Asilimia 35 walisema idadi ya wastani walijitokeza.

**Jedwali Na. 3.3: Mahudhurio ya Wananchi kwenye Kupata Elimu ya Mpiga Kura**

| Je, ni kwa kiasi gani wananchi walihudhuria utoaji wa elimu ya mpiga kura? | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| *Hakuna aliyehudhuria utaoaji wa elimu ya mpiga kura* | *Hakuna aliyehuhudhuria (%)* | *Mahudhurio hafifu (%)* | *Mahudhurio ya wastani (%)* | *Mahudhurio mazuri (%)* | *Jumla (%)* |

| (%) | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 41 (46) | 0 (0) | 6 (7) | 31 (35) | 11 (12) | 89 (100) |

Kama ilivyooneshwa katika Jedwali Namba 3.4, Tume ilitumia njia mbalimbali kufikisha elimu ya mpiga kura kwa umma. Zaidi ya nusu (asilimia 53) ya waangalizi wa TEMCO walisema kwamba matangazo ya redio yalitumika kutoa taarifa juu ya elimu ya uandikishaji wapiga kura na Tume ya Taifa ya Uchaguzi/Tume ya Uchaguzi Zanzibar. Hii inaonesha ni kwa kiasi gani redio zinawafikia wanachi, hususan wananchi wa maeneo ya vijijini kuliko vyombo vingine vya habari. Pamoja na matangazo ya redio, Tume ilitumia matangazo ya runinga, vipeperushi, magari ya sinema, matangazo ya magazeti, mafunzo ya uraia kwenye maeneo yenye mkusanyiko wa watu wengi kama vile masokoni na vituo vya mabasi, pamoja na mitandao ya kijamii.

**Jedwali Na. 3.4: Njia Zilizotumiwa na Tume kutoa Elimu ya Mpiga Kura**

| *Ni njia gani zilitumiwa na Tume kutoa elimu ya mpiga kura?* | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| *Tume haikutoa elimu ya mpiga kura (%)* | *Vipeperushi (%)* | *Matangazo ya magazeti (%)* | *Matangazo ya redio (%)* | *Matangazo ya runinga (%)* | *Mitandao ya kijamii (%)* | *Magari ya sinema (%)* | *Mafunzo ya uraia (%)* | *Nyingine (%)* | *Jumla (%)* |
| 10 (11) | 19 (21) | 5 (9) | 12 (13) | 24 (27) | 9 (10) | 9 (18) | 12 (13) | 46 (52) | 89 (100) |

Tume iliimarisha mkakati wake wa kutoa elimu ya mpiga kura kwa kutumia mitandao ya kijamii, hususan Instagram, WhatsApp na Facebook. Taarifa za kila wakati na taarifa husika kuhusu uboreshaji wa daftari la kudumu la wapiga kura ziliwekwa kwenye mitandao hii ya kijamii kwa wakati. Huu ni mkakati mzuri kwani, pamoja na kuboresha muonekano wa Tume, unasaidia kujenga imani miongoni mwa wapiga kura wanaostahili na wadau wengine wa uchaguzi kwani shughuli zinafanywa kwa uwazi. Lakini muhimu zaidi ni kwamba Tume ilifikia idadi kubwa ya wapiga kura wanaostahili, kama vijana ambao wengi wao wanatumia mitandao ya kijamii zaidi kuliko kundi jingine lolote lile katika jamii.

Zaidi ya nusu ya waangalizi wetu walisema kwamba walishuhudia au kusikia kuhusu shughuli za utoaji elimu ya mpiga kura zilizolenga kuongeza ushiriki wa makundi maalumu, yaani akina mama (asilimia 51), vijana (asilimia 52) na watu wenye ulemavu (asilimia 50) (tazama Jedwali Namba 3.5).

**Jedwali Na. 3.5: Utoaji wa Elimu ya Mpiga Kura kwa Makundi Maalumu**

| *Swali* | *Ndiyo, nilishuhudia (%)* | *Ndiyo, nilisikia (%)* | *Hapana (%)* | *Jumla (%)* |
|---|---|---|---|---|
| Umeshuhudia au kusikia kuhusu shughuli za utoaji elimu ya mpiga kura zilizokusudiwa kuongeza ushiriki wa akina mama katika Mamlaka ya Serikali ya Mtaa ulipofanya kazi? | 6 (7) | 39 (44) | 44 (49) | 89 (100) |
| Umeshuhudia au kusikia kuhusu shughuli za utoaji elimu ya mpiga kura zilizokusudiwa kuongeza ushiriki wa vijana katika Mamlaka ya Serikali ya Mtaa ulipofanya kazi? | 7 (8) | 39 (44) | 43 (48) | 89 (100) |
| Umeshuhudia au kusikia kuhusu shughuli za utoaji elimu ya mpiga kura zilizokusudiwa kuongeza ushiriki wa watu wenye ulemavu katika Mamlaka ya Serikali ya Mtaa ulipofanya kazi? | 6 (7) | 38 (43) | 45 (51) | 89 (100) |

Kama Jedwali Namba 3.5 linavyoonesha, elimu ya mpiga kura iliyotolewa na Tume ilikuwa ya ujumla na ililenga jamii nzima. Haikulenga kundi maalumu fulani au kundi la watu wenye mahitaji maalumu.

Aidha, TEMCO iliangalia utoshelevu wa elimu ya mpiga kura iliyotolewa na Tume na kwa ujumla iligundua kwamba haikujitosheleza. Magari ya kutoa elimu yalikuwa na manufaa kwa watu wanaoishi jirani na barabara kuu ambako magari hayo yalipita. Kwenye baadhi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa, kwa sababu taarifa ilikuwa inatolewa dakika za mwisho, magari hayo yalipita kwa haraka na kupelekea ujumbe usiwafikie walengwa ipasavyo. Watu walipewa nafasi finyu kuuliza maswali au kupata ufafanuzi. Iligundulika kwamba Tume haikutenga fedha za kutosha kwa ajili ya utolewaji wa elimu ya mpiga kura. Kwenye baadhi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ilibainika kwamba wasimamizi wa uchaguzi waliajiri vijana na kuwalipa shilingi 3,000 au 5,000 ili wazunguke na ngoma kuwahimiza watu waende wakajiandikishe. Katika Halmashauri ya Kilindi, TEMCO iliona njia ya kipekee ya kutoa elimu ya mpiga kura ambapo maafisa waandikishaji walitengeneza vipeperushi ambavyo walivigawa kwa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari. Njia hii ilifanya kazi na kupelekea ujumbe kuwafikia watu wengi.

## 4. UPATIKANAJI NA MAFUNZO KWA MAAFISA WAANDIKISHAJI

Tume iliajiri na kutoa mafunzo kwa maafisa waandikishaji wapiga kura kwenye kila Mamlaka ya Serikali ya Mtaa iliyoangaliwa. Kwenye kila Mamlaka ya Serikali ya Mtaa, Tume iliajiri maafisa wa kutosha walioendana na idadi ya vituo vya kuandikisha wapiga kura. Kwa kiasi kikubwa, kila kituo cha kuandikisha wapiga kura kilipaswa kuwa na walau maafisa wawili: Mtaalamu wa mashine ya BVR na Afisa Mwandikishaji Msaidizi. Hii ilikuwa na faida kwani ilihalalisha usambazaji wa watendaji ingawa TEMCO iligundua kuwa uhalalishaji huu ungeweza kutumiwa kuongeza idadi ya maafisa, hususan kwenye maeneo yenye watu wengi ambapo maafisa waandikishaji wapiga kura walizidiwa.

### 4.1 Upatikanaji wa Maafisa Waandikishaji

Waangalizi wengi wa TEMCO (asilimia 70) walisema kwamba maafisa waandikishaji wengi walikuwa watumishi wa umma. Maafisa wa kuandikisha wapiga kura wa ngazi mbalimbali (yaani ngazi ya mkoa na kata) waliteuliwa na Tume kulingana na vifungu 7A(1) na 8(1 &2) vya Sheria Namba 13 ya 2004 na Sheria Namba 8 ya 1995, kulingana na nafasi zao. Walikuwa wakurugenzi wa manispaa, miji na wilaya na watendaji wa kata. Lakini, kama Jedwali Namba 4.1 linavyoonyesha, kwa upande wa Zanzibar waangalizi wa TEMCO waligundua kwamba maafisa waandikishaji wengi hawakuwa watumishi wa umma, bali waliteuliwa kulingana na nafasi zao binafsi.

**Jedwali Na. 4.1: Maafisa Waandikishaji ambao ni Watumishi wa Umma**

| *Tanzania Bara na Zanzibar* | *Wacha che (%)* | *Wengi (%)* | *Wote (%)* | *Hakuna taarifa (%)* | *Jumla (%)* |
|---|---|---|---|---|---|
| Maafisha waandikishaji ambao ni watumishi wa umma (Bara) | 8 (10) | 60 (76) | 5 (6) | 6 (8) | 79 (100) |
| Maafisha waandikishaji ambao ni watumishi wa umma (Zanzibar) | 6 (60) | 2 (20) | 1 (10) | 1 (10) | 10 (100) |

Taarifa za waangalizi wa TEMCO pia zilionesha kuwa wanawake na watu wenye ulemavu wachache sana waliteuliwa kama wataalamu wa mashine za BVR. Kwa kiasi kikubwa, uteuzi ulizingatia uwezo wa mtu binafsi na sifa alizokuwa nazo, ikitegemea na usaili wa uteuzi uliofanyika.

## 4.2 Mafunzo kwa Maafisa Waandikishaji

Watoaji mafunzo kutoka Tume walipelekwa kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa kuwapa mafunzo waratibu wa kuandikisha wapiga kura wa mkoa, waandishi wasaidizi na wataalamu wa Tehama. Katika ngazi ya kata, waratibu wa kuandikisha wapiga kura wa mkoa walitoa mafunzo kwa maafisa waandikishi wasaidizi. Katika ngazi ya kata, waratibu wa kuandikisha wapiga kura wa mkoa walisaidiwa na maafisa waandikishi wasaidizi. Katika ngazi ya kata, maafisa waandishi wasaidizi walitoa mafunzo kwa maafisa waandishi katika ngazi ya kata na wataalamu wa mashine za BVR.

Mafunzo yalihusu sheria na kanuni zinazoongoza uandikishaji wapiga kura, pamoja na ujazaji wa Fomu Namba 1 kwa ajili ya kuandikisha wapiga kura wapya/kusahihisha taarifa za mpiga kura/kupotea au kuharibika kwa kitambulisho cha mpiga kura; na Fomu Namba 5B kwa ajili ya kufuta taarifa za mpiga kura. Walipewa mafunzo juu ya kugundua wapiga kura wanaostahili, namna ya kutumia mashine za BVR, haki za wapiga kura, waangalizi na mawakala wa vyama vya siasa.

Waangalizi 80 wa TEMCO (asilimia 90) walisema kuwa maafisa wa kuandikisha wapiga kura walipewa mafunzo kwa siku mbili. Ni waangalizi nane tu (asilimia 9) ndio waliosema kwamba mafunzo yalitolewa kwa zaidi ya siku mbili. Kwa asilimia kubwa mafunzo yalitolewa madarasani (kama waangalizi asilimia 94 walivyosema). Njia zingine ni mazoezi ya kutumia vifaa, mafunzo ya ana kwa ana, machapisho kuhusu mafunzo na michezo ya kuigiza michache (kama ilivyoripotiwa na waangalizi 20, yaani asilimia 22). Siku ya pili ilitumika kufanya mazoezi ya namna ya kutumia mashine za BVR.

**Jedwali Na. 4.2: Ruhusa ya Kuangalia Mafunzo ya Maafisa Waandishi**

| *Swali* | *Ndiyo (%)* | *Hapana (%)* | *Jumla* |
|---|---|---|---|
| Je, uliruhusiwa kuangalia mafunzo ya maafisa waandikishaji wapiga kura kituoni? | 83 (93) | 6 (7) | 89 (100) |

Kama ilivyooneshwa katika Jedwali Namba 4.2, waangalizi wote wa TEMCO waliruhusiwa kuangalia mafunzo ya waandishi, ispokuwa waangalizi wa Halmashauri ya Wilaya ya Njombe, Halmashauri ya Wilaya ya Songea, Halmashauri ya Wilaya ya Songea, Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba, Halmashauri ya Wilaya ya Nyasa, Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga, Halmashauri ya Wilaya ya Iringa, Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa na Halmashauri ya Wilaya ya ChakeChake Zanzibar, ambao hawakuruhusiwa kuangalia mafunzo ya siku ya kwanza. Waliambiwa na maafisa waandishi wapiga kura husika kuwa hawaruhusiwi kuhudhuria mafunzo hayo. Lakini

waliruhusiwa kuhudhuria mafunzo ya siku ya pili baada ya mawasiliano kati ya Sekretarieti ya TEMCO na makao makuu ya Tume.

## 5. MCHAKATO WA KUANDIKISHA WAPIGA KURA

Baada ya kuingia eneo la kazi na kuangalia shughuli za awali kabla ya zoezi la kuandikisha wapiga kura halijaanza, pamoja na utoaji wa elimu ya mpiga kura, utafutaji na utoaji mafunzo kwa maafisa waandikishaji wapiga kura, waangalizi wa TEMCO walianza kuangalia mchakato wenyewe wa kuandikisha wapiga kura. Muhimu zaidi ni kwamba TEMCO iliangalia kipindi cha kuandikisha wapiga kura kwenye kila Mamlaka ya Serikali ya Mtaa, muda wa kufungua na kufunga vituo vya kuandikisha wapiga kura, mazingira ya ujumla kwenye vituo vya kuandikisha wapiga kura, umahiri wa maafisa waandikishaji wapiga kura na taratibu za kiusalama.

### 5.1 Ufunguzi wa Vituo vya Kuandikisha Wapiga Kura na Utoshelevu wa Vifaa

Katika kila Mamlaka ya Serikali ya Mtaa wapiga kura waliandikishwa kwa siku saba, isipokuwa kwa Dar es Salaam ambako kwa sababu ya wingi wa watu waliohitaji kuandikishwa Tume iliongeza siku tatu ili kukamilisha zoezi hilo. Kila kituo cha kuandikisha wapiga kura kilipaswa kufunguliwa saa mbili kamili asubuhi na kufungwa saa kumi na mbili jioni. Kwa kiasi kikubwa hili lilizingatiwa.

**Jedwali Na. 5.1: Ufunguzi wa Vituo vya Kuandikisha Wapiga Kura**

| *Kituo cha kuandikisha wapiga kura kilifunguliwa saa ngapi?* | | | |
|---|---|---|---|
| *Hadi 8.00 asubuhi (%)* | *Saa 8.00 asubuhi hadi saa 4.00 asubuhi (%)* | *Baada ya saa 6.00 mchana (%)* | *Jumla (%)* |
| 476 (78) | 137 (22) | | 614 (100) |

Kati ya vituo 614 vilivyoangaliwa, vituo 476 (asilimia 78) vilifunguliwa kwa wakati, yaani saa mbili kamili asubuhi. Vituo vilivyobaki 137 (asilimia 22) vilifunguliwa kati ya saa 2.00 asubuhi na saa 4.00 asubuhi (tazama Jedwali Namba 5.1).

Ni vituo vichache sana ambavyo vilichelewa kufunguliwa, kwa mfano kituo cha Majengo, Mbeya, ambapo mtaalamu wa mashine ya BVR alichelewa kwa dakika kumi, akimwambia afisa mwandikishaji wapiga kura msaidizi kwamba alichelewa kwa sababu ya foleni barabarani ambayo ilisababishwa na wanajeshi ambao walikuwa wanafanya mazoezi katika kata husika. Lakini hali hii haikuathiri zoezi la kuandikisha wapiga kura kwani hakuna mtu ambaye alikuwa ameshawasili kituoni kwa ajili ya kujiandikisha. Afisa huyu alionywa na kukumbushwa umuhimu wa kuwahi.

**Jedwali Na. 5.2: Jinsia ya Maafisa Waandikishaji**

| *Swali* | *Kiume (%)* | *Kike (%)* | *Jumla (%)* |
|---|---|---|---|
| Je, afisa mwandikishaji alikuwa mwanaume au mwanamke? | 308 (50) | 306 (50) | 614 (100) |

Tume ilizingatia jinsia katika kuajiri. Kulikuwa na tofauti ndogo sana kati ya wanaume na wanawake miongoni mwa maafisa waandikishaji (tazama Jedwali Namba 5.2). Taarifa zinaonesha kwamba wengi wa wataalamu wa mashine za BVR walikuwa wanaume. Wanawake wengi walikuwa waandishi wasaidizi.

## 5.2 Utoshelevu wa Vifaa vya Kuandikishia

TEMCO ilibaini kwamba vifaa vya kuandikishia vilikuwa vya kutosha, isipokuwa kwenye vituo vichache vya kuandikisha wapiga kura ambapo baadhi ya vifaa vilikuwa vinakosekana (tazama Jedwali Namba 5.3). Vituo vya kuandikisha wapiga kura vilikuwa na vifaa vya kutosha; vilikuwa na mashine za BVR na fomu za maombi ya kujiandikisha. Lakini TEMCO iligundua kuwa vituo vingi (asilimia 79) havikuwa na mashine ya BVR za ziada (tazama Jedwali Namba 5.3).

Katika baadhi ya vituo, TEMCO iligundua kuwa hapakuwa na maandalizi ya kutosha kwa ajili ya usafi, viti, meza, vyoo, umeme na vifaa vingine muhimu ili zoezi ambalo linawaleta watu wengi pamoja liende vizuri.

**Jedwali Na. 5.3: Uwepo wa Vifaa vya Kuandikisha Wapiga Kura**

| *Swali* | *Ndiyo (%)* | *Hapana (%)* | *Jumla (%)* |
|---|---|---|---|
| Kituo kilikuwa na mashine za BVR? | 614 (100) | 0 (0) | 614 (100) |
| Kituo kilikuwa na mashine za ziada za BVR? | 127 (21) | 487 (79) | 614 (100) |
| Kituo kilikuwa na fomu za maombi ya kuandikisha wapiga kura? | 606 (99) | 8 (1) | 614 (100) |

**Jedwali Na. 5.4: Ulinganisho wa Uwepo wa Mashine za BVR za Ziada**

| *Kituo kilkuwa na mashine za BVR za ziada?* | *Ndiyo (%)* | *Hapana (%)* | *Jumla (%)* |
|---|---|---|---|
| **Tanzania Bara** | **127 (21)** | **487 (79)** | **614 (100)** |
| Kanda ya Kati | 2 (6) | 33 (94) | 35 (100) |
| Kanda ya Pwani | 57 (25) | 172 (75) | 229 (100) |
| Kanda ya Kusini | 32 (20) | 129 (80) | 161 (100) |
| Kanda ya Nyanda za Juu Kusini | 19 (16) | 100 (84) | 119 (100) |

| | | | |
|---|---|---|---|
| Zanzibar | 17(24) | 53 (76) | 70 (100) |

Jedwali Namba 5.5 linaonesha uwepo na hali za kamera zilizokuwapo na zilizokuwa zinafanya kazi.

**Jedwali Na. 5.5: Uwepo na Hali ya Kamera**

| *Swali* | *Ndiyo, ilikuwa inafanya kazi (%)* | *Ndiyo, lakini haikuwa inafanya kazi (%)* | *Hapana (%)* | *Jumla (%)* |
|---|---|---|---|---|
| Je, kituo cha kuandikisha wapiga kura kilikuwa na kamera? | 611 (100) | 3 (0) | 0 (0) | 614 (100) |

## 5.3 Mipango ya Kiusalama

Usalama ni muhimu sana kwenye zoezi lenye maslahi ya kitaifa kama uandikishaji wapiga kura. Amani na utulivu ulikuwa muhimu kipindi chote cha kuandikisha wapiga kura. Waangalizi wa TEMCO walingundua kwamba karibu kila mtu aliyekuwapo kwenye kituo cha kuandikisha wapiga kura alikuwa ameidhinishwa (tazama Jedwali Namba 5.6). Kwa mshangao, wanaangalizi wa TEMCO waliokuwepo kwenye mikoa mitatu ya kanda ya kusini (Lindi, Mtwara na Ruvuma) hawakuona afisa usalama yeyote kwenye vituo vya uandikishaji. Ilitarajiwa maafisa usalama kuwepo kwenye vituo vilivyopo kwenye mikoa ya mpakani, hususan Mtwara na Ruvuma ambapo raia wa kigeni wanavuka mpaka mara kwa mara na kujumuika na wakazi wa maeneo hayo.

**Jedwali Na. 5.6: Kama Watu Wasioruhusiwa walikuwepo kwenye Vituo vya Kuandikisha Wapiga Kura**

| *Swali* | *Ndiyo (%)* | *Hapana (%)* | *Jumla (%)* |
|---|---|---|---|
| Je, alikuwapo mtu yeyote ambaye hakuidhinishwa kwenye kituo cha kuandikisha wapiga kura wakati wa maandalizi? | 3 (0) | 611 (100) | 614 (100) |

**Jedwali Na. 5.7: Uwepo wa Maafisa Usalama**

| *Je, walikuwapo maafisa usalama waliovaa sare katika kituo cha kuandikisha wapiga kura?* | *Ndiyo (%)* | *Hapana (%)* | *Jumla (%)* |
|---|---|---|---|
| **Tanzania Bara** | **12 (2)** | **602 (98)** | **614 (100)** |
| Kanda ya Kati | 1 (3) | 34 (97) | 35 (100) |
| Kanda ya Pwani | 4 (2) | 225 (98) | 229 (100) |
| Kanda ya Kusini | 0 (0) | 161 (100) | 161 (100) |
| Kanda ya Nyanda za Juu Kusini | 4 (3) | 115 (97) | 119 (100) |

| | | | |
|---|---|---|---|
| Zanzibar | 3 (4) | 67 (96) | 70 (100) |

### 5.4 Ufanisi wa Maafisa Waandikishaji

TEMCO ilitaka kuangalia kama maafisa waandikishaji walikuwa na uwezo wa kufanya kazi kwa ufanisi na weledi. TEMCO ililinganisha muda uliotumika kumwandikisha mpiga kura mmoja katika kituo fulani na kulinganisha muda huo na vituo vingine. Muda wa kuandikisha wapiga kura ulitofautiana. Katika baadhi ya maeneo ilichukua dakika tano na mpaka dakika 20 katika maeneo mengine.

Kwa wastani, utendaji wa wataalamu wa mashine za BVR ulikuwa wakutosha katika vituo asilimia 94 kati ya vituo vyote vilivyoangaliwa. Ufanisi katika utendaji ulionekana Zanzibar ambako vituo vyote 70 vya kuandikisha wapiga kura vilivyoangaliwa vilikuwa na maafisa mahiri (tazama Jedwali Namba 5.8). Hii ni kwa sababu watu wenye uwezo waliajiriwa na maafisa waandikishaji wapiga kura walipewa mafunzo ya kutosha. Katika moja ya vituo vya kuandikisha wapiga kura mjini Njombe, mtaalamu wa mashine ya BVR alikuwa anapiga simu mara kwa mara ili kumsaidia mtaalamu wa mashine kama hiyo wa kituo kingine ambaye ilionekana alikuwa anakabiliwa na ugumu katika kutumia mashine hiyo.

Kwenye maeneo yaliyo mengi, siku ya kwanza wataalamu wa mashine za BVR walifanya kazi taratibu, lakini kadiri zoezi la kuandikisha wapiga kura lilivyoendelea walizidi kuzielewa mashine na kasi ya kuandikisha iliongezeka. Waliowahi kufanya kazi kama hiyo siku za nyuma walikuwa na ufanisi mkubwa, ufahamu mkubwa na kasi kubwa kuliko wale walioshiriki kwa mara kwanza. Maafisa waandikishaji wapiga kura wa Unguja Kusini walishindwa kuandika vizuri majina ya watu wa kutoka Tanzania Bara ambao walikuwa Zanzibar na walitaka kujiandikisha. Hii ilisababisha ucheleweshaji kwa sababu baadhi ya watu waliotaka kujiandikisha waliombwa waandike majina yao kwenye vipande vya karatasi, na hata hivyo baadhi ya majina bado yalikosewa.

**Jedwali Na. 5.8: Ufanisi katika Kutumia Mashine za BVR**

| *Je, maafisa waandikishaji wapiga kura wa Tume walionekana kujua namna ya kutumia mashine za BVR?* | *Ndiyo (%)* | *Hapana (%)* | *Jumla (%)* |
|---|---|---|---|
| **Tanzania Bara** | **576 (94)** | **38 (6)** | **614 (100)** |
| Kanda ya Kati | 35 (100) | 0 (0) | 35 (100) |
| Kanda ya Pwani | 224 (98) | 5 (2) | 229 (100) |
| Kanda ya Kusini | 146 (91) | 15 (9) | 161 (100) |
| Kanda ya Nyanda za Juu Kusini | 101 (85) | 18 (94) | 119 (100) |

| | | | |
|---|---|---|---|
| Zanzibar | 70 (100) | 0 (0 | 70 (100) |

## 5.5 Utendaji Kazi wa Mashine za BVR na Uandikishaji wa Wapiga Kura

TEMCO iliangalia utendaji kazi wa mashine za BVR ili kubaini kama ziliharibika mara kwa mara, kitu ambacho kingeathiri ubora wa zoezi la kuandikisha wapiga kura na kuwanyima watu waliostahili kuandikishwa nafasi ya kupiga kura. Katika hatua hii, TEMCO pia iliangalia uandikishaji halisi wa wapiga kura. TEMCO ilitaka kufahamu ni kwa namna gani maafisa waandikishaji wapiga kura waliwahudumia watu ambao walikuwa wanajiandikisha kwenye daftari la kudumu la wapiga kura.

Kama ilivyooneshwa katika Jedwali Namba 5.9, katika vituo vya kuandikisha wapiga kura 137 (asilimia 22) mashine za BRV ziliharibika. Mashine za BVR ziliharibika zaidi katika kanda ya kati (asilimia 29) kuliko kwenye kanda nyingine ukilinganisha na Zanzibar ambako mashine ziliharibika mara chache sana (asilimia 14). Muda ambao mashine ziliharibika ulikuwa tofauti kati ya dakika chache hadi saa kadhaa. Kwa mfano, walikuwapo waatalamu wa tehama wachache sana makao makuu Namtumbo. Hivyo, iliwachukua wataalamu hao muda mrefu kwenda vijijini kutatua matatizo. Siku ya tarehe 4 Januari 2020 mshine ya BVR ya kituo cha kuandikisha wapiga wapiga kura cha Skuli ya Finya iliharibika kwa sababu ya umeme kuwa mdogo. Mashine zilichajiwa Wete kwa sababu hazikuwapo mashine za BVR za ziada na jitihada za kuwasiliana na makao makuu ya wilaya hazikufanikiwa.

**Jedwali Na. 5.9: Kuharibika kwa Mashine za BVR**

| *Je, kuna wakati wowote ambao mashine ziliharibika au kushindwa kufanya kazi?* | *Ndiyo (%)* | *Hapana (%)* | *Jumla (%)* |
|---|---|---|---|
| **Tanzania Bara** | **137 (22)** | **477 (78)** | **614 (100)** |
| Kanda ya Kati | 10 (29) | 25 (71) | 35 (100) |
| Kanda ya Pwani | 54 (24) | 175 (76) | 229 (100) |
| Kanda ya Kusini | 38 (24) | 123 (76) | 161 (100) |
| Kanda ya Nyanda za Juu Kusini | 25 (21) | 94 (79) | 119 (100) |
| Zanzibar | 10 (14) | 60 (86) | 70 (100) |

TEMCO iligundua kwamba karibu nusu ya wapiga kura walioandikishwa (asililimia 46) hawakuombwa kutoa uthibitisho wa kustahili kuandikishwa kabla hawajaandikishwa (tazama Jedwali Namba 5.10). Wapiga kura zaidi waliombwa kutoa uthibitisho wa kustahili kwao kuandikishwa Zanzibar (asilimia 83) kuliko maeneo mengine ya Tanzania (asilimia 43). Masheha walikuwapo kwenye kila kituo cha kuandikisia wapiga kura Zanzibar. Jukumu lao lilikuwa kuthibitisha ukazi wa watu waliotaka kujiandikisha na kwa hiyo ilikuwa rahisi kubaini watu ambao hawakustahili kuandikishwa.

Iligundulika kwa mshangao mkubwa katika baadhi ya vituo vya kuandikisha wapiga kura Mbeya maafisa waandikishaji wapiga kura walimrudisha mtu yeyote aliyekwenda kujiandikisha akiwa amevaa fulana yenye kola ya duara. Haikufahamika mara moja agizo hili lilitoka wapi kwa sababu kitu hicho hakikufanyika kwenye vituo vingine.

**Jedwali Na. 5.10: Uthibitisho wa Kustahili Kuandikishwa**

| *Je, kila mwombaji aliombwa kutoa uthibitisho wa kustahili kuandikishwa?* | *Ndiyo (%)* | *Hapana (%)* | *Jumla (%)* |
|---|---|---|---|
| **Tanzania Bara** | **262 (43)** | **282 (46)** | **614 (100)** |
| Kanda ya Kati | 19 (54) | 16 (46) | 35 (100) |
| Kanda ya Pwani | 120 (52) | 109 (48) | 229 (100) |
| Kanda ya Kusini | 70 (43) | 91 (57) | 161 (100) |
| Kanda ya Nyanda za Juu Kusini | 53 (45) | 66 (55) | 119 (100) |
| Zanzibar | 58 (83) | 12 (17) | 70 (100) |

Zilikuwapo taarifa nyingi za kupotea au kuharibika kwa vitambulisho vya mpiga kura. Kam Jedwali Namba 5.11 linavyoonesha, asilimia 88 ya wapiga kura walikuwa na tatizo hili. Hili lilijitokeza zaidi kanda ya kusini na kanda ya nyanda za juu kusini (asilimia 98 na 97). Watu wachache sana wa Zanzibar walikuwa na tatizo hili (asilimia 41).

**Jedwali Na. 5.11: Upotevu wa Vitambulisho vya Wapiga Kura**

| *Je, zilikuwapo kesi zozote za upotevu au kuharibika kwa vitambulisho vya wapiga kura katika vituo vya kuandikisha wapiga kura?* | *Ndiyo (%)* | *Hapana (%)* | *Jumla (%)* |
|---|---|---|---|
| **Tanzania Bara** | **541 (88)** | **73 (12)** | **614 (100)** |
| Kanda ya Kati | 32 (91) | 3 (9) | 35 (100) |
| Kanda ya Pwani | 206 (90) | 23 (10) | 229 (100) |
| Kanda ya Kusini | 158 (98) | 3 (2) | 161 (100) |
| Kanda ya Nyanda za Juu Kusini | 116 (97) | 3 (3) | 119 (100) |
| Zanzibar | 29 (41) | 41 (59) | 70 (100) |

Kwa ujumla, TEMCO ilibaini kwamba hakuna mtu aliyeruhusiwa kujiandikisha kwa niaba ya mtu mwingine (tazama Jedwali Namba 5.12).

**Jedwali Na. 5.12: Kujiandikisha kwa Niaba ya Mtu Mwingine**

| *Swali* | *Ndiyo (%)* | *Hapana (%)* | *Jumla (%)* |
|---|---|---|---|
| Je, kuna mtu yeyote ambaye aliruhusiwa kujiandikisha kwa niaba ya mtu mwingine? | 1 (0) | 613 (100) | 614 (100) |

Kwa ujumla, katika vituo ambavyo TEMCO iliviangalia zoezi lilifanyika kwa amani. Ni vituo nane tu ambapo vitisho na bugudha zilijitokeza (tazama Jedwali Namba 5.13). Matukio hayo nane ya vitisho na bugudha yalijitokeza Manispaa ya Kinondoni (mara moja), Temeke (mara tatu), Kibaha Mjini (mara moja), Jijini Tanga (mara moja) na Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya (mara mbili). Yafuatayo ni baadhi ya matukio yaliyosimuliwa na waangalizi wa TEMCO:

a) Manispaa ya Kinondoni: Mwombaji mmoja alichukua kwa nguvu fomu iliyokuwa imejazwa vibaya kutoka kwa afisa mwandikishaji wapiga kura ambaye alitaka kuitunza fomu hiyo kama ushahidi kwamba ilikuwa imejazwa lakini vibaya. Utulivu ulirudi baada ya afisa mwandikishaji msaidizi wa kata kufika na kutishia kuwaita polisi.
b) Manispaa ya Temeke: Watu waliokuwa kwenye mstari kwa ajili ya kujiandikisha walikerwa na maafisa waliokuwa wanafanya kazi kwenye ofisi za mtendaji kata ambao walijifanya kuwa maafisa waandikishaji wapiga kura na kuanza kuwahudumia watu waliowafahamu badala ya wale ambao walikuwa kwenye mstari.
c) Kibaha Mjini: Vijana watatu kutoka kata ya Kwa Mfipa walirudishwa na mtendaji kata na wakala wa CCM na waliombwa walete barua kuthibitisha mahali wanakoishi. Walikataa na kuanza kuwarushia maneno mtendaji kata na wakala wa CCM. Palikuwa na foleni ndefu kwenye kata ya Kwa Mfipa.
d) Jijini Tanga: Baada ya kuombwa atoe taarifa zake binafsi, mpiga kura mmoja ambaye alikuwa anajiandikisha alikuwa mkali kwa mtaalamu wa mashine za BVR, akimsemea maneno mabaya na kuelezea kutopendezwa kwake na swali hilo.
e) Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya: Mtaalamu wa mashine ya BVR alikuwa na hasira na hakutoa ushirikiano ambao kila mtu aliupenda, hususan kwa watu ambao walikuwa wanasubiri taarifa zao zichukuliwe kwa ajili ya kujiandikisha. Mtaalamu alitoa majibu makali.

**Jedwali Na. 5.13: Vitisho na Bugudha**

| *Je, kuna wakati wowote ambao mtu yeyote alijaribu kuwatisha, kubughudhi au kuwajeruhi maafisa waandikishaji wapiga kura, waombaji, wawakilishi wa vyama vya siasa na waangalizi?* | | | |
|---|---|---|---|
| | *Ndiyo (%)* | *Hapana (%)* | *Jumla (%)* |
| **Tanzania Bara** | **8 (1)** | **606 (99)** | **614 (100)** |
| Kanda ya Kati | 0 (0) | 35 (100) | 35 (100) |
| Kanda ya Pwani | 6 (3) | 223 (99) | 229 (100) |

| | | | |
|---|---|---|---|
| Kanda ya Kusini | 0 (0) | 161 (100) | 161 (100) |
| Kanda ya Nyanda za Juu Kusini | 2 (2) | 117 (98) | 119 (100) |
| Zanzibar | 0 (100) | 70 (100) | 70 (100) |

Usitishaji wa zoezi la kuandikisha wapiga kura haukujitokeza sana na ulionekana kwenye vituo 79 kati ya vituo vyote vilivyoangaliwa (asilimia 13) (tazama Jedwali Namba 5.14). Ukilinganisha na maeneo mengine, kanda ya pwani ilikuwa na matukio mengi ya kusitisha kuandikisha wapiga kura. Matukio haya yanaweza kuwekwa katika makundi matatu, kama ifuatavyo:

a) Kuharibika kwa mashine za BVR:
   - Kuharibika kwa kamera na mashine za kuchapa;
   - Upungufu wa wino;
   - Upungufu wa chaji kwenye mashine za BVR.

b) Upungufu wa fomu za kuandikishia wapiga kura (hususan Fomu Namba 1) na vitambulisho vya wapiga kura; na

c) Kutokuwapo kwa muda kwa wataalamu wa mashine za BVR au kushindwa kutekeleza majukumu yao:
   - Mtaalamu mmoja wa mashine za BVR alichukulia ukaribu wa kituo cha kuandikisha wapiga kura na nyumbani kwake ambako aliienda kupata chakula cha mchana (badala ya kuomba chakula kiletwe kituoni);
   - Mtaalamu mwingine wa mashine za BVR alikwenda msikitini kwa ajili ya sala ya Ijumaa;
   - Afisa mwandikishaji mmoja aliugua ghafla na kupelekea zoezi kusitishwa. Zoezi la kuandikisha wapiga kura liliendelea alipopata nafuu.

**Jedwali Na. 5.14: Usitishaji wa Zoezi la Kuandikisha Wapiga Kura**

| *Je, uandikishaji wapiga kura ulisitishwa wakati wowote wakati wa uandikishaji?* | *Ndiyo (%)* | *Hapana (%)* | *Jumla (%)* |
|---|---|---|---|
| **Tanzania Bara** | **79 (13)** | **535 (85)** | **614 (100)** |
| Kanda ya Kati | 6 (17) | 29 (83) | 35 (100) |
| Kanda ya Pwani | 21 (9) | 208 (91) | 229 (100) |
| Kanda ya Kusini | 19 (12) | 142 (88) | 161 (100) |
| Kanda ya Nyanda za Juu Kusini | 16 (13) | 103 (94) | 119 (100) |
| Zanzibar | 17 (24) | 53 (76) | 70 (100) |

## 5.6 Mahali na Urahisi wa Kuvifikia Vituo vya Kuandikisha Wapiga Kura

Katika kuhakikisha zoezi la kuandikisha wapiga kura linafanikiwa, Tume inapaswa kuhakikisha usalama wa watu na vifaa, na kufikika na kukubalika kwa vituo vya kuandikisha wapiga kura. Kwa hiyo, sheria inataka uandikishaji wapiga kura ufanyike kwenye majengo ya umma.

Jedwali Namba 5.15 linaonesha kwamba vituo vya kuandikisha wapiga kura (558 au asilimia 91) viliwekwa kwenye majengo ya umma. Pale ambapo majengo ya umma hayakuwapo au hayakutosha, Tume ilitumia vituo vya muda. TEMCO ilishuhudia vituo 29 vya aina hiyo (asilimia 5). Kwa asilimia kubwa vituo hivyo vilitengenezwa kwa kutumia maturubai maalumu yaliyotolewa na Tume kwenye maeneo maalumu. Kwa ujumla, vituo vyote vya kuandikisha wapiga kura vilikuwa kwenye majengo ya umma kwa upande wa Zanzibar. Kanda ya pwani ilikuwa na vituo vingi vya muda kuliko kanda zingine.

**Jedwali Na. 5.15: Sehemu Vilipokuwepo Vituo vya Kuandikisha Wapiga Kura**

| *Kituo cha kuandikisha wapiga kura kiliwekwa sehemu gani?* | *Jengo la umma (%)* | *Sehemu ya ibada (%)* | *Jengo la muda (%)* | *Nyingine (%)* | *Jumla (%)* |
|---|---|---|---|---|---|
| **Tanzania Bara** | **558 (91)** | **1 (0)** | **29 (5)** | **26 (4)** | **614(100)** |
| Kanda ya Kati | 32 (91) | 1 (3) | 1 (3) | 1 (3) | 35 (100) |
| Kanda ya Pwani | 205 (90) | 0 (0) | 10 (4) | 14 (6) | 229(100) |
| Kanda ya Kusini | 146 (91) | 0 (0) | 6 (4) | 9 (6) | 161 (100) |
| Kanda ya Nyanda za Juu Kusini | 105 (88) | 0 (0) | 12 (10) | 2 (2) | 395 (100) |
| Zanzibar | 70 (100) | 0 (0) | 0 (0) | 0 (0) | 70 (100) |

Baadhi ya vituo vya kuandikisha wapiga kura vilikabiliwa na changamoto kama mafuriko, kwa mfano mvua kubwa iliponyesha katika *Zahanati ya Itensa*, katika Halmashauri ya Jiji la Mbeya, siku ya tarehe 8 Desemba 2019. Hali hii ilipelekea mtendaji kata awabebe maafisa waandikishaji wapiga kura na vifaa vya kuandikishia kwenye gali lake baada ya zoezi kufungwa saa kumi na mbili jioni.




*Kwenye picha ya kushoto: Kituo cha kuandikisha wapiga kura cha Zahanati ya Itensa kabla mvua haijaanza kunyesha na picha ya upande wa kushoto inaonesha kituo hicho kikiwa kimezungukwa na maji saa kumi na moja jioni, Halmashauri ya Jiji la Mbeya, 8 Desemba 2019*.

Kituo cha "Kwa Mzee Mwasanga" ni mfano wa kituo cha kuandikisha wapiga kura cha muda. Iliponyesha mvua kubwa kituo kilikuwa hatarini kuzolewa kwa sababu watu waliojenga kituo hawakutumia misumari kukiimarisha. Baada ya mvua kumalizika, hema lilizungukwa na tope na kusababisha usumbufu kwa maafisa wa kuandikisha wapiga kura na wananchi waliojitokeza kwa ajili ya kuandikishwa. Usalama wa vifaa vya kuandikishia pia ulikuwa mashakani.



*Afisa mwandikishaji wapiga kura msaidizi akichukua taarifa za mwananchi aliyeomba kitambulisho kipya cha mpiga kura na mtaalamu wa mashine ya BVR anampiga picha mwananchi mwingine ambaye alikwenda kuandikishwa kwenye daftari la kudumu la wapiga kura. Picha inaonesha eneo la ndani la kituo cha kuandikisha wapiga kura cha Kwa Mzee Mwasanga kikiwa na tope jingi baada ya mvua kubwa kunyesha, Mtaa wa Nkuyu, Kata ya Iganzo, Halmashauri ya Jiji la Mbeya, 11 Desemba 2019*.



*Mvua zilisababisha ugumu kwa watu na vifaa kusafirishwa kutoka sehemu moja hadi nyingine kama picha ya hapo juu iliyopigw Halmashauri ya Wilaya ya Kilindi inavyoonyesha*



*Maafisa waandikishaji wapiga kura wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa wakifanya jitihada ya kukifikia kituo cha kuandikisha wapiga kura baada ya mvua kubwa kunyesha.*

Majengo hayakukusudiwa kwa ajili ya kuandikisha wapiga kura; kwa hiyo, katika baadhi ya maeneo uandikishaji ulifanyika kwenye baraza za nyumba au kwenye wodi tupu za zahanati. Aidha, baadhi ya majengo ya umma yalijengwa zamani kipindi ambapo kanuni za ufikiwaji, hususan kwa watu wenye ulemavu, hazikuwapo. Kama Jedwali Namba 5.16 linavyoonyesha, ni asilimia 50 tu ya vituo vya kuandikisha wapiga kura vilivyoangaliwa viliweza kufikiwa kwa urahisi na watu wenye ulemavu.

**Jedwali Na. 5.16: Ufikiwaji wa Vituo vya Kuandikisha Wapiga Kura**

| Je, kituo kinaweza kufikiwa na watu wenye ulemavu? | *Kabisa (%)* | *Kiasi (%)* | *Hapana (%)* | *Jumla (%)* |
|---|---|---|---|---|
| **Tanzania Bara** | **310 (50)** | **228 (37)** | **76 (12)** | **614 (100)** |
| Kanda ya Kati | 9 (26) | 24 (69) | 2 (6) | 35 (100) |
| Kanda ya Pwani | 82 (36) | 82 (36) | 2 (6) | 229 (100) |
| Kanda ya Kusini | 96 (60) | 46 (29) | 19 (12) | 161 (100) |
| Kanda ya Nyanda za Juu Kusini | 73 (61) | 39 (33) | 7 (6) | 119 (100 |
| Zanzibar | 50 (71) | 19 (27) | 1 (1) | 70 (100) |




*Baadhi ya vituo vya kuandikisha wapiga kura kama hiki cha Mikindani Mtwara havikuweza kufikiwa na watu wenye ulemavu.*

## 5.7 Ushiriki wa Vyama vya Siasa

Kama wadau wakuu, ushiriki wa vyama vya siasa ni muhimu kwa mafanikio na kuaminika kwa mchakato wowote wa uchaguzi. Kwa hiyo, sheria zinaruhusu vyama vya siasa kuweka mawakala wao kwenye vituo vya kuandikisha wapiga kura kama wanapenda. Jedwali Namba 5.17 linaonyesha kuwa vyama vya siasa viliweka mawakala wachache sana na ni kwenye baadhi ya maeneo tu. Ni vyama vinne tu vya siasa ambavyo viliweka mawakala kwenye vituo vya kuandikisha wapiga kura: CCM iliweka mawakala kwenye vituo 262 (asilimia 43), ACT-Wazalendo kwenye vituo 56 (asilimia 9), CUF kwenye vituo 20 (asilimia 3) na CHADEMA kwenye vituo 30 (asilimia 5).

**Jedwali Na. 5.17: Mawakala wa Vyama vya Siasa kwenye Vituo vya Kuandikisha Wapiga Kura**

| *Ni vyama vipi vya siasa viliweka mawakala kwenye vituo vya kuandikisha wapiga kura?* | *Hakuna wakala wa chama cha siasa (%)* | *CCM (%)* | *CHADEMA (%)* | *CUF (%)* | *ACT-Wazalendo (%)* | *Jumla (%)* |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Tanzania Bara** | **340 (55)** | **262(43)** | **30 (5)** | **20(3)** | **56 (9)** | **614(100)** |
| Kanda ya Kati | 34 (97) | 1 (3) | 0 (0) | 0 (0) | 0 (0) | 35 (100) |
| Kanda ya Pwani | 77 (34) | 151 (66) | 14 (6) | 1 (0) | 1 (0) | 229 (100) |
| Kanda ya Kusini | 133 (83) | 28 (17) | 0 (0) | 0 (0) | 1 (1) | 161 (100) |
| Kanda ya Nyanda za Juu Kusini | 88 (74) | 31 (26) | 4 (3) | 0 (0) | 0 (0) | 119 (100) |
| Zanzibar | 8 (11) | 51 (73) | 12 (17) | 1(27) | 54(77) | 70 (100) |

## 5.8 Kushirikiana na Waangalizi wa TEMCO

Kanuni za uchaguzi zinataka waangalizi wa uchaguzi waidhinishwe na wapewe ushirikiano na mafisa uchaguzi ili waweze kufanya shughuli zao. Kama ilivyooneshwa kwenye Jedwali Namba 5.18, waangalizi wa TEMCO walipata ushirikiano wa kutosha kutoka kwa maafisa wa Tume kwenye vituo vya kuandikisha wapiga kura na wote waliruhusiwa kuangalia uandikishaji wapiga kura.

**Jedwali Na. 5.18: Kuzuia Uangalizi**

| *Swali* | *Ndiyo (%)* | *Hapana (%)* | *Jumla (%)* |
|---|---|---|---|
| Je, kuna muda wowote ambao ulizuiwa kuangalia uandikishaji wapiga kura, pamoja na kunyimwa taarifa za msingi kuhusu mchakato huo? | 2 (0) | 612 (100) | 614 (100) |
| Ulishuhudia waangalizi ambao siyo wa TEMCO au mawakala wa vyama vya siasa wakizuiwa kuangalia uandikishaji wapiga kura? | 1 (0) | 613(100) | 614 (100) |

## 5.9 Kufunga Vituo vya Kuandikisha Wapiga Kura

Vituo vya kuandikisha wapiga kura vilipaswa kufungwa saa kumi na mbili jioni kama wote waliokuja kujiandikisha walikuwa wameandikishwa. Katika vituo vingi

vilivyoangaliwa hali ilikuwa hivyo. TEMCO ilibaini kwamba vituo 14 vya kuandikisha wapiga kura vilifungwa kabla vya saa 12 jioni (tazama Jedwali Namba 5.19). Kwa mfano, kitu hiki kilitokea kwenye Sheha moja Unguja Kusini ambako zoezi la kujiandikisha lilisitishwa saa 10 jioni. Afisa alidai kwamba ilikuwa ni kawaida kwa maafisa waandikishaji wapiga kura kuandikisha watu waliosimama kwenye mstari mapema ili wapate muda wa kuweka sawa data zao.

**Jedwali Na. 5.18: Muda wa Kufunga Vituo vya Kuandikisha Wapiga Kura**

| *Kituo cha kuandikisha wapiga kura kilifungwa kabla ya saa 12 jioni?* | *Ndiyo (%)* | *Hapana (%)* | *Jumla (%)* |
|---|---|---|---|
| **Tanzania Bara** | **21 (3)** | **593 (97)** | **614 (100)** |
| Kanda ya Kati | 0 (0) | 35 (100) | 35 (100) |
| Kanda ya Pwani | 8 (3) | 221 (97) | 229 (100) |
| Kanda ya Kusini | 2 (1) | 159 (98) | 161 (100) |
| Kanda ya Nyanda za Juu Kusini | 2 (2) | 117 (98) | 119 (100) |
| Zanzibar | 9 (35) | 61 (87) | 70 (100) |

Kama Jedwali Namba 5.20 linavyoonesha, vifaa vya kuandikisha wapiga kura vilitunzwa kwa uangalifu kila siku baada ya zoezi la kuandikisha wapiga kura kufungwa.

**Jedwali Na. 5.20: Utunzaji wa Vifaa vya kuandikisha Wapiga Kura**

| *Swali* | *Ndiyo (%)* | *Hapana (%)* | *Jumla (%)* |
|---|---|---|---|
| Vifaa vyote vya kuandikisha vilitunzwa baada ya kumalizika kwa zoezi la uandikishaji? | 606 (99) | 8 (1) | 614(100) |

## 6. HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

### 6.1 Hitimisho

Kwa kiasi kikubwa zoezi la kuandikisha wapiga kura lilifanyika kwa mafanikio makubwa kwenye Mamlaka zote 89 za Serikali ya Mtaa zilizoangaliwa na TEMCO. Tume ilifanya maandalizi yote ya utaratibu, pamoja na kuandaa ratiba kwa ajili ya kuandikisha wapiga kura katika nyakati tofauti nchi nzima. Kwa kiasi kikubwa, vifaa vya kuandikishia wapiga kura vilikuwa vya kutosha na vilisambazwa kwa wakati. Uajiri, utoaji mafunzo na usambazaji wa maafisa waandikishaji wapiga kura ulifanyika kwa namna ambayo wadau wengi, ikiwa ni pamoja na TEMCO, waliridhika.

Tume ilitoa elimu ya mpiga kura kwa kiasi kikubwa. Wadau wengine, pamoja na asasi za kiraia na vyama vya siasa, hawakushiriki sana kwenye utoaji wa elimu hiyo. Kazi hii

kubwa iliipa Tume mzigo mkubwa. Matumizi ya mitandao ya kijamii yalikuwa maarufu na yenye manufaa. Magari yaliyopita kutoa elimu kwa jamii na vipeperushi ni miongoni mwa njia kuu zilizotumika kutoa elimu ya mpiga kura. Njia hizi zilikuwa na mapungufu na katika baadhi ya maeneo TEMCO iliwaona wapiga kura tarajiwa wakiomba ufafanuzi kutoka kwa maafisa waandikishaji wapiga kura, na kwa hiyo kuwaongezea mzigo ukizingatia walikuwa na muda finyu wa kufanya kazi.

Watalaamu wa Tehama walifanya kazi nzuri ya kuhakikisha kwamba mashine za BRV zinafanya kazi kwa kiwango cha juu. Pia walikuwapo na walikuwa tayari kutatua matatizo yote ya kiufundi yaliyojitokeza wakati wa kuandikisha wapiga kura. Lakini, kutokana na kuharibika kwa mashine hizo, kuna wakati walishindwa kuvifikia vituo vingi, na kusababisha ucheleweshaji au kusitishwa kwa zoezi la kuandikisha wapiga kura kwa muda. Suala ambalo lilijitokeza mara kwa mara ambalo waangalizi wa TEMCO waliliona ni lile la kuharibika kwa mashine za BVR, yaani kifaa cha BVR, mashine za kuchapa, kompyuta na kamera. Miongoni mwa masuala yote yaliyoangaliwa na waangalizi kama masuala makubwa kila siku, walau moja wapo lilihusu mambo ya kiufundi ya kutumia na kufanya kazi kwa mashine za BRV. Kuharibika mara kwa mara kwa mashine za BVR, mashine za kuchapa na kamera na kutofanya kazi kwa kompyuta ni mambo ambayo yalijitokeza kwenye vituo vichache, na hii ilipelekea kuhairishwa kwa zoezi la kuandikisha wapiga kura. Kwenye maeneo ambayo zoezi lilisitishwa kwa zaidi ya saa moja, baadhi ya waombaji waliondoka bila kuandikishwa na hapakuwa na uhakika kwamba wangerudi tena siku ya pili kwa ajili ya kujiandikisha.

Matukio machache ya upungufu au kuchelewa kwa vifaa muhimu vya kuandikisha wapiga kura kwenye Halmashauri zilizoangaliwa na vituo vya kuandikisha wapiga kura husika. Pia, kulikuwa na upungufu wa fomu za maombi. TEMCO ilishuhudia ucheleweshaji wa vifaa vya kuandikisha wapiga kura Zanzibar ambavyo vilisafirishwa kwa meli kutoka Tanzania Bara. Utaratibu wa kupata hati ya kuruhusu zipite katika bandari ya Zanzibar ulicheleweshа ufunguaji wa vituo vya kuandikisha wapiga kura. Tukio kubwa sana ni kuchelewa kwa vifaa kutoka Tume kwenda mikoa ya Njombe na Ruvuma; hali hii ilipelekea zoezi liairishwe kwa siku mbili.

Vituo vingi sana havikuwa na walinzi. Ingawa hapakuwa na matukio ya vurugu yaliyoonesha ulazima wa kupeleka vyombo vya usalama, shughuli kama hizi ni muhimu zifanyike pakiwa na ulinzi. Hii ni changamoto kwa Tume na Serikali kuhakikisha kwamba michakato ya kuandikisha wapiga kura ya miaka ijayo na masuala ya uchaguzi mengine yanafanyika pakiwa na ulinzi, walau askari mmoja kwa kila kituo.

## 6.2 Mapendekezo

TEMCO inapenda kuambatisha kwenye taarifa hii mapendekezo ambayo yatasaidia kuongeza ufanisi na mafanikio ya zoezi la kuandikisha wapiga kura siku za usoni:

(i) Vipindi vya redio vianze kutumika muda mrefu kabla zoezi la kuandikisha wapiga kura halijaanza ili kutoa elimu ya mpiga kura. Njia nyingine, hususan matumizi ya magazeti, mitandao ya kijamii, maoni na viongozi wa kidini, zitakuwa na manufaa pia.

(ii) Kuongeza utoaji na vile vile muonekano wa vipindi vya elimu ya mpiga kura mahsusi kwa makundi maalum, yaani wanawake, vijana na watu wenye ulemavu. Jitihada za Tume, halmashauri, asasi, vyama vya siasa, na wadau wengine zinazohamasisha jamii ili kuhakikisha wanakuwa na uelewa, ufahamu, utayari, na uwezo wa kushiriki kikamilifu kwenye mchakato wa uchaguzi zitilie maanano maslahi ya makundi maalum yaliyotajwa hapo juu, hususan wanawake na watu wenye ulemavu.

(iii) Kuhusu elimu ya uraia, ambayo elimu ya uraia ni sehemu yake, kuna haja ya kuweka bayana mamlaka inayotoa vibali, vigezo vya asasi na taasisi zinazoitoa, ugharamiaji na hatua za udhibiti wa ubora.

(iv) Idadi ya wataalamu wa tehama iongezwe ili kuhakikisha kwamba kila mmoja anahudumia idadi ya vituo ambayo anaimudu.

(v) Bado ni changamoto kwa Tume kuzishawishi asasi za kiraia ambazo zimesajiliwa kutoa elimu ya uraia kipindi cha kuandikisha wapiga kura.

(vi) Kuvishirikisha na kuvikumbusha vyama vya siasa kuweka mawakala wa vyama katika vituo vya kuandisha wapiga kura.

(vii) Maafisa usalama wapelekwe kwenye vituo vya kuandikisha wapiga kura ili kuhakikisha usalama, utulivu na amani.

(viii) Pawepo na mashine za BVR za ziada. Hii itapunguza baadhi ya malalamiko kutoka kwa watu ambao husubiri kwa muda pindi mashine zinapoharibika.

(ix) Kutokana na ripoti ya idadi kubwa ya kadi zilizopotea na zilizoharibika, Tume izidishe na kuelekeza kampeni yake ya kuelimisha wapiga kura walioandikishwa ili wahakikishe wanatunza vitambulisho vyao vya mpiga kura. Wapiga kura walioandikishwa wahakikishe vitambulisho vyao havihariki, kupotea au kuchukuliwa bila ridhaa zao.

(x) Kuendelea kuwapa kipaumbele wakina mama wajawazito na wenye watoto wachanga, wagonjwa, vikongwe na watu wenye ulemavu.

(xi) Wito kwa Tume kuimarisha mfumo wake wa mawasiliano ili kuwezesha ufikishaji, kwa wakati mzuri, wa taarifa muhimu, maamuzi na matukio yanayohusiana na mchakato wa uchaguzi. TEMCO inatambua maboresho

makubwa katika mfumo wa mawasiliano wa Tume kupitia taarifa za mara kwa mara za kwenye tovuti, blog, mitandao ya kijamii kama Instagram, NEC Online Tv kwenye YouTube na mikutano na wahandihsi wa habari, lakini kwa bahati mbaya TEMCO haikufahamishwa mapema kuhusu mabadiliko ya ratiba ya uandikishaji, kwa mfano kwa Zanzibar na baadhi ya Halmashauri za Morogoro na kuongezwa jwa muda wa uandikishaji kwa mkoa wa Dar es Salaam, hivyo TEMCO haikuweza kubadili mpango wa kuwapeleka waangalizi wake ambao walishafika kwenye halmashauri walizopangiwa.

**KIAMBATISHO I: MAENEO AMBAYO UANGALIZI WA TEMCO ULIFANYIKA**

| KANDA | MKOA | HALMASHAURI/MIJI |
|---|---|---|
| Kati | Dodoma | Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino |
| | | Dodoma Jiji |
| | | Halmashauri ya Wilaya ya Bahi |
| | | Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa |
| | | Halmashauri ya Wilaya Mpwapwa |
| | | |
| Nyanda za Juu Kusini | Mbeya | Halmashauri ya Wilaya ya Kyela |
| | | Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya |
| | | Mbeya Jiji |
| | | Halmashauri ya Wilaya ya Busokelo |
| | | Halmashauri ya Wilaya ya Chunya |
| | | Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali |
| | | Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe |
| | | |
| | Iringa | Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi |
| | | Halmashauri ya Mji Mafinga |
| | | Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo |
| | | Halmashauri ya Wilaya ya Iringa |
| | | Halmashauri ya Manispaa ya Iringa |
| | | |
| | Njombe | Halmashauri ya Wilaya ya Njombe |

| | | |
|---|---|---|
| | | Njombe Mji |
| | | Makambako Mji |
| | | Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa |
| | | Halmashauri ya Wilaya ya Wanging'ombe |
| | | |
| Kusini | Ruvuma | Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo |
| | | Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga |
| | | Mbinga Mji |
| | | Halmashauri ya Wilaya ya Nyasa |
| | | Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru |
| | | Halmashauri ya Manispaa ya Songea |
| | | Halmashauri ya Wilaya ya Madaba |
| | | Halmashauri ya Wilaya ya Songea |
| | | |
| | Lindi | Halmashauri ya Wilaya ya Nachingwea |
| | | Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa |
| | | Halmashauri ya Wilaya ya Liwale |
| | | Halmashauri ya Manispaa ya Lindi |
| | | Halmashauri ya Wilaya ya Lindi |
| | | Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa |
| | | |
| | Mtwara | Halmashauri ya Wilaya ya Newala |

| | | |
|---|---|---|
| | | Halmashauri ya Mji wa Newala |
| | | Halmashauri ya Wilaya ya Nanyumbu |
| | | Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara |
| | | Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara |
| | | Nanyamba Mji |
| | | Halmashauri ya Wilaya ya Masasi |
| | | Masasi Mji |
| | | Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba |
| | | |
| Pwani | Dar es Salaam | Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni |
| | | Ilala Jiji |
| | | Halmashauri ya Manispaa ya Ilala |
| | | Halmashauri ya Manispaa ya Temeke |
| | | Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni |
| | | Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo |
| | | |
| | Pwani | Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo |
| | | Halmashauri ya Wilaya ya Chalinze |
| | | Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga |
| | | Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji |
| | | Halmashauri ya Wilaya ya Mafia |
| | | Halmashauri ya Wilaya ya |

| | | |
|---|---|---|
| | | Kibaha |
| | | Kibaha Mji |
| | | Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe |
| | | Halmashauri ya Wilaya ya Kibiti |
| | | |
| | Morogoro | Halmashauri ya Wilaya ya Gairo |
| | | Halmashauri ya Wilaya ya Kilombero |
| | | Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero |
| | | Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro |
| | | Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro |
| | | Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa |
| | | Ifakara Mji |
| | | Halmashauri ya Wilaya ya Ulanga |
| | | Halmashauri ya Wilaya ya Malinyi |
| | | |
| | Tanga | Tanga Jiji |
| | | Halmashauri ya Wilaya ya Muheza |
| | | Halmashauri ya Wilaya ya Mkinga |
| | | Halmashauri ya Wilaya ya Pangani |
| | | Halmashauri ya Wilaya ya Handeni |
| | | Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe |
| | | Halmashauri ya Wilaya ya Kilindi |

| | | |
|---|---|---|
| | | Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto |
| | | Halmashauri ya Wilaya ya Bumbuli |
| | | |
| Zanzibar | KaskaziniUnguja | Mjini Magharibi 'A' |
| | | Mjini Kaskazini 'B' |
| | KusiniUnguja | Kusini |
| | MjiniMagharibi | Mjini |
| | | Mjini Magharibi |
| | | Kati |
| | Kaskazini Pemba | Wete |
| | | Micheweni |
| | Kusini Pemba | ChakeChake |
| | | Mkoani |